JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BIHARAMULO

SHULE YA SEKONDARI NYAKAHURA,
S.L.P 193,
BIHARAMULO.

Namba ya simu
Mkuu wa shule: 0768453828
Makamu wa shule: 0744185685
Msajiri: 0752557952
Matron:0621167552/ 0763503233
Patron 0765091862

Mzazi/mlezi wa mwanafunzi

……

S.L.P ……..

……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYAKAHURA HALMASHAURI YA BIHARAMULO MKOA KAGERA MWAKA 2021

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2021 katika tahasusi ya HGK/HGL/HGE/HKL/CBG. Shule ya Sekondari Nyakahura ipo umbali wa kilometa 75 magharibi mwa mji wa biharamulo, usafiri wa mabasi kutoka mjini Biharamulo unapatikana katika kituo cha mabasi Biharamulo kwa nauli ya tsh 6000/=
Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe ……. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe …….. na mwisho wa kuripoti ni tarehe……..

Mambo muhimu ya kuzingatia.

1. **SARE ZA SHULE**
   A. WASICHANA
   - DARASANI

(i) Sketi nyeusi mshono wa linda box kubwa **mbele** na **nyuma** inayofika juu ya kisigino. au suruari isiyobana kwa wasichana wa kiislamu (Hijjabu) kama ilivyoambatanishwa nyuma ya fomu hii.
(ii) Shati mbili nyeupe za mikono mirefu aina ya Tetron (unatakiwa uje nayo kutoka nyumbani).

Edit with WPS Office

(iii) Viatu vya ngozi nyeusi jozi mbili vyenye kamba visivyo na kisigino kirefu na visiwe na urembo wowote
(iv) Soksi ndefu nyeupe
(v) Sweta rangi ya kijani lenye alama ya V shingoni lenye nembo ya shule.
(vi) Tishet ya kola rangi Nyekundu yenye nembo ya shule TSH 15000 na itavaliwa siku ya jumatano na siku nyingine ni baada ya kutoka darasani
(vii) Hijjabu kwa wasichana wa Kiislamu, Rangi ya Hijjab ifanane na sare ya shule.
(viii) Tai ya pundamilia nyeusi na nyeupe TSH 5000

-NJE YA DARASA

(i) Gauni 1 rangi ya damu ya mzee (maruni) kitambaa cha sukarisukari,sketi 1 rangi ya damu ya mzee(kitambaa kizito)
(ii) Hijjabu 2 na ushungi/mtandio rangi ya damu ya mzee(maruni) kwa wasichana wa kiislamu.

B. WAVULANA
-DARASANI

(i) Suruali nyeusi (yenye marinda mawili kila upande) kama ilivyo ambatanishwa nyuma ya fomu hii. **HAIRUHUSIWI KUVAA SURUALI ZA MODO SHULENI au aina yoyote ile ya nguo isiyo sare ya shule.**
(ii) Shati mbili nyeupe za mikono mirefu
(iii) Viatu vya ngozi nyeusi vya kamba jozi mbili.
(iv) Soksi nyeusi
(v) Sweta rangi ya kijani lenye alama ya V shingoni lenye nembo ya shule

-NJE YA DARASA

(i) Suruali 2 za kushindia kitambaa rangi ya damu ya mzee (maruni)
(ii) Tisheti ya kola rangi nyekundu yenye nembo ya shule.

Vifaa vya malazi, chakula na usafi:-

(i) Mopa, softbloom,jembe na kwanja kwa wasichana.
(ii) Mopa, kwanja,jembe na Mifagio migumu (hard broom) ya plastic kwa wavulana
(iii) Godoro la ft $2^1/_2$,Sahani, Bakuri, kikombe na kijiko kwa ajili ya chakula
(iv) Ndoo mbili za plastic lita 20 moja ya matumizi yake binafsi na moja ya shule
(v) Beseni
(vi) Mwanafunzi lazima aje na Chandarua
(vii) Blanketi - Ni muhimu kuja nayo.
(viii) Shuka mbili za rangi ya pinki.
(ix) Rim 1 A_4
(x) Toilet paper – 10 (mhula wa kwanza 5) ni lazima kwa matumizi binafsi
(xi) Taulo za kike za kutosha
(xii) DAWA YA CHOONI LITA 5
(xiii) Ili kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa COVID 19 mwanafunzi anashauriwa kuja na Barakoa.

Edit with WPS Office

(xiv) Tochi ya betrii/Solata
(xv) Faili moja la kawaida (folder file)

N.B vilevile kuna maduka karibu na shule ambapo vifaa vinapatikana kama vile ; **godoro kwanja, mopa, soft bloom, hard bloom, jembe ndoo, , sahani, bakuli, kikombe, kijiko, beseni, chandarua, toilet paper, rim, mathematical set na dawa ya chooni. Pia sweta, tisheti yenye nembo ya shule na tai vinapatikana shuleni.**

Vifaa vya masomo:-

(i) Daftari 5 kubwa kwa kuanzia (Counter book)
(ii) Daftari 10 ndogo kwa ajili ya majaribio ya mwezi.
(iii) Kalamu ya wino-bluu au nyeusi
(iv) Mfuko wa vitabu (school bag).
(v) Mathematical set
(vi) Dictionary
(vii) Mwanafunzi aje na kitabu kimojawapo katika masomo ambayo amechaguliwa orodha ya vitabu imeambatanishwa.
(viii) Wanafunzi watakao soma hesabu, kemia, uchumi na geografia waje na scientific calculator ambayo inakubalika katika ufundishaji yaani yenye **FUNCTION YA 991,**vilevile zinapatikana karibu na shule kwa tsh 45,000/=
(ix) Dissecting kit (kwa wanafunzi wa CBG)

Vifaa vya michezo

Utatakiwa kuwa na vifaa vya michezo vifuatavyo, ili kuvitumia wakati wa michezo mbalimbali hapa shuleni na nje ya shule.

(i) Viatu vya raba
(ii) Bukta mbili kwa wavulana rangi ya bluu/nyeundu
(iii) Track kwa wasichana rangi ya bluu/nyekundu(jezi)
(iv) Fulana (T-shirt) rangi ya bluu/nyekundu(jezi)

Ada na michango ya shule:-

(a). Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/= kwa mwanafunzi wa bweni na unaweza kulipa shilingi 35,000/= kwa muhula mmoja au kulipa yote kwa mara moja. Fedha zilipwe kwenye akaunti ya shule na. **31701200096 (nyakahura secondary school recurrent akaunti**) katika benki ya NMB (tafadhari andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).

(b). Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

(i) Tshs 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha
(ii) Tsh 20,000/= kwa ajili ya taaluma
(iii) Tshs 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
(iv) Tshs 2,000/= kwa ajili ya nembo ya shule
(v) Tshs 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza,kila mwanafunzi anapaswa kuwa na bima ya afya NHIF AMBAYE HANA atatakiwa kulipia 50,400/= ili awezekukatiwa BIMA hiyo ,shule haitagharimikia matibabu ya mwanafunzi

Edit with WPS Office

mgonjwa asiye na BIMA kwa uzembe wake mwenyewe. Hivyo ni lazima kila mwanafunzi kuwa na bima ya NHIF

(vii Tshs 20,000/= kwa ajili ya mitihani endelezi

(X) Tshs 5,000/= tahadhari(haitarejeshwa)

(xi) Tsh 25,000/= Ukarabati

Michango hiyo ilipwe kwenye akaunti hii **NYAKAHURA SECONDARY SCHOOL RECURRENT 31701200096.(NMB).**

NB. KILA MWANAFUNZI AJE BENK PAY IN SLIP INAYOONYESHA MICHANGO HIYO. (IKIWA NA MAJINA MATATU YA MWANAFUNZI ANAYELIPIWA ADA)

NAZIDI KUWAKUMBUSHA KUWA MKIWEKA MICHANGO HIYO KWENYE BENK ANDIKA NA JINA LA ALIYETUMA FEDHA HIZO.

Sheria na kanuni muhimu za shule hii:-

Shule inaendeshwa, kwa mujibu wa sheria ya elimu Na 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Pamoja na fomu hii ya kujiunga na shule, naambatanisha sheria za shule hii.

FOMU ZITAKAZORUDISHWA SHULENI NI PAMOJA NA;

a. Fomu ya uchunguzi wa afya “Medical examination form” ambayo itajazwa na mganga Mkuu wa Hospitali ya serikari. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
b. Fomu ya kuandikishwa shuleni, pamoja na ahadi ya mzazi/mlezi.
c. Nakala ya cheti cha kuzaliwa/ living certificate na result slip ni lazima

NB.

Uongozi wa shule unakutakia maandalizi mema na safari njema ya kuja hapa shuleni.

NACHUKUA NAFASI HII TENA KUKUPONGEZA NA KUKUKARIBISHA .

Wako katika Ujenzi wa Taifa

…….
BRAISON R. UHAKULA (MKUU WA SHULE)
SIMU 0768453828

Edit with WPS Office

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI

SHULE YA SEKONDARI NYAKAHURA

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Sheria za shule zinatungwa kufuatana na maadili ya Taifa letu. Lengo ni kutoa mwongozo na msaada kwa mwanafunzi ambaye anatarajia awe raia na mzalendo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Utii wa sheria za shule ni utii wa sheria za Taifa letu. Shule imepewa jukumu la kulea na kuelimisha vijana ili badaye wawe raia wema wa Taifa hili. Sharti mwanafunzi kufuata kanuni na sheria za shule.

Zifutazo ni sheria za shule na kila mwanafunzi anatakiwa aziheshimu na kuzizingatia ipasavyo:-

1. Mwanafunzi sharti aweheshimu walimu, wafanyakazi wote wa shule ambao ni walezi wake. Ajiepushe na lugha chafu, utovu wa nidhamu kwa walezi hawa pamoja na wanafunzi wenzake. Inampasa mwanafunzi kusimama sawa anapomwona mwalimu au mfanyakazi na mgeni na yeyote yule ambaye anamzidi umri na kumuamkia ipasavyo.
2. Ni kosa kubwa kwa mwanafunzi kukataa kufanya kazi za shule, au adhabu ya mwalimu au kiongozi yoyote yule wa wanafunzi aliyechaguliwa kwa mujibu wa sheria.
3. Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vya darasani na nje alivyopangiwa kwa wakati uliopangwa. Ni kosa kubwa kukosa vipindi bila sababu maalum.
4. Nimarufuku mwanafunzi kutoka nje ya mipaka ya shule isipokuwa kwa kibali maalumu cha mkuu wa shule. Kila mwanafunzi atawajibika kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
5. Kila mwanafunzi atalazimika kuzingatia ratiba ya siku nzima na kuitekeleza ”Daily Routine”
6. Kila mwanafunzi analazimika kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa shule na nje ya shule.
7. Kila mwanafunzi analazimika kuhudhuria maandalizi ya jioni (Night Preparation)
8. Ni lazima mwanafunzi ajiepushe na makosa ambayo yanaweza kusababisha afukuzwe shule.

- Wizi
- Uasherati, ubakaji na ushoga.
- Ulevi na matumizi mabaya ya dawa za kulevya.
- Uvutaji wa bangi.
- Makosa ya jinai
- Kupigana au kupiga
- Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

Edit with WPS Office

- Kudharau Bedera ya Taifa na picha za viongozi wakuu wa serikali.
- Kuoa au kuolewa.
- Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
- Kutoa mimba.
- Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu.
- Kukataa adhabu makusudi.
- Kuwa na simu ya mkononi
- Kuvaa suruari aina ya modo shuleni
- Kutohudhuria kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa
- Kujihusisha/kushiriki matendo ya uharifu siasa na matendo yeyote yale yanayovunja sheria za nchi
- Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kuua

9. Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalumu:-
    - Ofisi za shule
    - Maabara
    - Jikoni
    - Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu

10. Ni marufuku kwa mwanafunzi kutembelea sehemu zifuatazo:-
    - Vilabu vya pombe
    - Majumba ya starehe
    - Majumba ya kufikia wageni.
11. Ni marufuku wanafunzi kuvaa kofia, viatu vya ghorofa(viatu vyenye kisigino kirefu) na mapambo mengine mfano herein, vidani, mikufu na bangili Nk.
12. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kufanya usafi wa mazingira pamoja na usafi wake binafsi. Nywele ndefu haziruhusiwi; hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi kuhakikisha nywele zake ni fupi.

JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI

SHULE YA SEKONDARI – NYAKAHURA.

Edit with WPS Office

FOMU YA KUANDIKISHWA–SHULE

(Ijazwe kwa herufi kubwa na irejeshwe kwa mkuu wa shule)

1. Jina kamili……..

   Tarehe ya kuzaliwa…… Wilaya……..Mkoa……..……

   Taifa……..Dini:RC/Anglican/Lutheran/Muslim/Pentecoste/n.k……...

   Shule ya sekondari uliyomalizia(kidato cha nne)……..

2. Jina la Baba/Mama/Mlezi…….…..
   Anwani yake…….

   Kazi ya Baba/Mama/Mlezi……..

   Namba ya simu…….…….

AHADI YA MWANAFUNZI.

(a) Mimi……..nimeyasoma na kuyaelewa maelekezo yote ambayo ni pamoja na sheria na kanuni za shule na nimekubali kuingia kidato cha tano katika shule ya sekondari Nyakahura kuanzia tarehe…….hadi nitakapo maliza kidato cha sita.

(b) Kwa hiyo naahidi kwamba:-

- (i) Nitazitii sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa
- (ii) Sitashiriki vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na uongozi wa serikali ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania.
- (iii) Nitatunza mali ya umma ambayo ni pamoja na majengo, samani, vitabu n.k.

Tarehe ……sahihi ya mwanafunzi……..

AHADI YA MZAZI/MLEZI.

Mimi …….…….ambye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi…….ninahaidi kwamba:-

Edit with WPS Office

1. Nitashirikiana na uongozi wa shule, walimu na watumishi wasio walimu katika kuhakikisha, mwanangu anatii sheria na kanuni za shule ya sekondari Nyakahura na iwapo atashindwa kutii sheria hizo, nitalazimika kukubaliana na uamuzi utakaofanywa na uongozi wa shule.

2. Nitafanya kila niwezalo kumwezesha mwanangu, kusoma kwa kulipa Ada na michango mingine kama ilivyoelekezwa na shule.

Tarehe……

Sahihi…….Namba ya simu:……

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SHULE YA SEKONDARI NYAKAHURA,

S.L.P. 193,

BIHARAMULO.

MGANGA MKUU WA MKOA/ WILAYA/KITUO CHA AFYA

Edit with WPS Office

JINA(mwanafunzi) ……..amechaguliwa kujiunga na kidato cha ……katika shule hii, ili kuendelea na masomo ni lazima apimwe kwanza.

Nitafurahi iwapo mbali na kupimwa kijana huyu ataangaliwa uwezo wa kuona macho yake. Kama imeshauriwa avae miwani hana budi kuinunua yeye mwenyewe kwa fedha yake .

Tafadhari nijazie sehemu inayohusika chini baada ya kupima.

Ahsante kwa ushirikiano

Nimempima mwanafunzi aliyetajwa hapo juu nakuona kwamba ana /hana matatizo/ugonjwa wa;

A. Kifua kikuu…….
B. Macho……
C. Masikio……..
D. Akili…….
E. Kilema chochote……..
F. Choo……
G. Kwa wasichana tu nimeona ana/hana mimba…….
H. Athma……..
I. Mengineyo……
J. Maoni ya mganga ……

SAINI NA MHURI WA OFISI……

MGANGA MKUU WA MKOA/WILAYA/KITUO CHA AFYA…….

Edit with WPS Office



PICHA YA SKETI JINSI INAVYOTAKIWA KUSHONWA

Edit with WPS Office

ORODHA YA VITABU

	SOMO	-JINA LA KITABU
1,	CHEMISTRY	-A-LEVEL CHEMISTRY
		-PHYSICAL CHEMISTRY
		-INORGANT CHEMISTRY
2	BIOLOGY	-BIOLOGICAL SCIENCE
		-NEW UNDERSTANDING BIOLOGY
3	HISTORY	-HISTORY PAPER II ALIVE
		-SALEH YASINHISTORY 1 AND 2
		-SHIBITALI CIC TUMAIN HISTORY 1 AND 2
4	GEOGRAPHY	-MONKHOUSE (PHYSICAL GEOGRAPHY)
		-GEOGRAPHY INTERGRATED
5	ECONOMICS	-ECONOMICS SIMPLIFIED
		-MODERN ECONOMICS
		-MICRO ECI=ONOMICS
6	KISWAHILI	-KISWAHILI (NADHARIA YA LUGHA KIDATO CHA 5 AND 6
		-KISWAHILI 2 NADHARIA YA FASIHI KIDATO CHA 5 AND 6
		-TAFSIRI NA UKALIMANI
7	BAM	-PURE AND APPLIED
		-ADV MATH 1
8	GENERAL STUDIES	-GENERAL STUDIES NOTES
		-GENERAL STUDIES SUPPLEMENTARY BOOK FOR A-LEVEL
9	ENGLISH	-ADVANCED ENGLISH LANGUAGE FORM 5 AND 6
		-BETRAYAL IN THE CITY
		-I WILL MARY WHEN I WANT
		-AN ENEMY OF THE PEOPLE
		--A MAN OF THE PEOPLE
		-THE BEUTYFUL ONES ARE NOT YET BORN
		-DIVINE PROVIDENCE

NB. **MWANAFUNZI APATE KITABU KIMOJA KILA SOMO, KITABU HIKI NI MALI YA MWANAFUNZI MEWENYEWE**.

Edit with WPS Office